**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA MUSOMA.**

S.L.P 128
**Musoma**
13/05/2026

Namba za **Simu:**
**Mkuu wa shule 0767677660**
**Makamu Mkuu wa Shule 0784251795**
**Mwalimu wa Taaluma 0684423982**

**E-mail:morembesec@musomamc.go.tz**

*Fomu Namba ………………………...*

**Kumb. Na. MRDSS/MSM/J3/VOL I/11/2026**
Ndugu Mzazi/mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………
S.L.P …………………………………
……………………………..

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MOREMBE, HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA, MKOA WA MARA MWAKA……………………..**

**1.0 Utangulizi**

Nina furahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii na atasoma tahasusi ………………..

Shule ya Sekondari **Morembe** ipo umbali wa kilomita nane (8) mashariki mwa mji mkuu wa mkoa/**Halmashauri ya Manispaa ya Musoma**. **Shule hii ni ya Bweni Wasichana kwa kidato cha Tano na sita.** Usafiri wa Pikipiki au Bajaji kutoka stand ya mabasi Bweri hadi shuleni umbali wa kilometa moja(1km)unapatikana kwa nauli ya Tsh: 1,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **……………….** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **……………….** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **…………………………**

### 1.1 Mambo muhimu ya kuzingatia

### 1.11 Sare ya Shule

- Sketi mbili nyeusi kitambaa kizito “original” zenye michirizi miwili mieupe yenye upana wa inchi moja (1) mbele ya sketi. Usawa wa kitovu, michirizi itenganishwe kwa inchi moja na nusu (1.5) iwe na marinda na ivaliwe/ifungwe tumboni, iwe ni yenye urefu unaofika katika vifundo vya miguu.
- Shati nyeupe mbili (2) mikono mirefu isiyo bana mwili (kitambaa cha tetron)
- Tai ndefu na iwe nyeusi (ziwe 2)
- Sweta rangi ya kijivu iwe na muundo wa V – shape shingoni na Tshirt ya shule kijani jeshi yenye kola. inapatikana shuleni kwa Tsh: 15,000/= pesa hiyo unakuja nayo shuleni na kukabidhiwa Tshirt uliyolipia.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) siyo “stockings”
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na kisigino kifupi
- Picha mbili (2) za “passport size”
- Nguo za kushindia ni sketi dark blue yenye malinda ya kawaida na Tshirt rangi damu ya mzee.
- Mwanafunzi aje na taulo za kike za kutosha.
- Godoro la kulalia mwanafunzi futi 2.5 kwa sita kuanzia inchi 3’’
- Shuka mbili rangi ya blue bahari, pilo(mto wa kulalia) na net(chandarua) rangi nyeupe ya pembe nne.
- Taulo ya kuogea na ndala, ndoo ya lita kumi (10) ya kuogea
- Tochi ya kutumia wakati wa giza.



**NB: Usithubutu kushona sketi ya mitindo ya solo, taiti, rinda boksi, kimini pia mwanafunzi haruhusiwi kuwa na mavazi ya kanga, kitenge na mitandio ya aina yoyote.**

**Wanafunzi wasichana wa Kiislamu sare yao ni;**

**1. Sketi**

- Iwe ni yenye urefu unaofika katika vifundo vya miguu
- Iwe pana na isiwe nyepesi

**2. Blauzi (Nusu Kanzu)**

- Iwe ya mikono mirefu isiyofunika viganja vya mikono

- ➢ Iwe pana (isibane)
- ➢ Iwe ndefu inayoshuka chini ya makalio ( isiwe kama gauni)
- ➢ Isiwe nyepesi

**3. Kitambaa cha kichwani (Ushungi)**

- ➢ Kiwe kipana cheupe na ndani kitambaa cheusi
- ➢ Kiwe kirefu kisichofunika viganja vya mikono
- ➢ Kisifunike uso na kisiwe chepesi

**NB: Vazi lingine la aina yoyote litakalovaliwa kinyume na maelekezo yaliyopo hapo juu halitatambuliwa kuwa ni "Hijab"**

**1.12 Nguo za michezo shuleni**

- ✓ Wasichana wanatakiwa kuvaa bukuta na tsheti rangi ya bluu na raba za michezo na vitakaguliwa kama vinakidhi vigezo.
- ✓ Track suit ni rangi ya blue isiyobana zenye kola.

**2.0. Sheria na kanuni muhimu za shule**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu - **TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi mara baada ya kuripoti shuleni.

**MAMBO YA KUZINGATIA UWAPO SHULENI**

**<u>SHERIA NA KANUNI ZA SHULE</u>**

Shule hii inaendeshwa kwa mujib wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.

**2.1 Mambo ya kuzingatia:**

Shule ya Sekondari Morembe ni mahali wanapoishi walimu, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi. Hivyo unatakiwa kutambua na kuheshimiana.

**A. HESHIMA**

i) Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.

ii) Kusimama na kumsalimu mwalimu, Mzazi au Kiongozi anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

iii) Kutumia **LUGHA NZURI** ya ya heshima mahali popote kwa mtu yeyote.

iv) Kuheshimu bendera ya Taifa, Picha za Viongozi wa NCHI, Nembo ya Taifa (Court of Army), Fedha na wimbo wa Taifa.

v) Kuheshimu Ofisi za Shule, ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, mali za umma na mali binafsi zilizopo katika mazingira ya Shule.

vi) Kusimama kwenye mstari wakati wa kupokea huduma. Mwanafunzi akimbie na kuwahi anaposikia wito wa dharura.

vii) Kukubali na kuheshimu tofauti za KIDINI, KISIASA NA KIUTAMADUNI katika jamii. Mwanafunzi haruhusiwi kuhubiri dini, siasa au jambo lolote Shuleni. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile Kanisani, Msikitini na katika vipindi vya dini vilivyopangwa kwenye ratiba ya Shule.

**B. RATIBA YA SHULE**

i) Mwanafunzi awepo shuleni saa moja kamili asubuhi. Mwanafunzi anatakiwa kukaa darasani Muda wote wa vipindi na kutimiza wajibu na kazi alizopewa.

**C. MIPAKA YA SHULE**

i) Mwanafunzi aifahamu vizuri mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu kuwepo ndani ya mipaka hiyo au nje ya mipaka hiyo kwa kibali maalum wakati wote. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea/kuingia kwenye nyumba za starehe, vilabu vya pombe na nyumba za kufikia wageni.

**D. USAFI**

i) Kutunza usafi wa mwili; Nywele fupi njiti ya kiberiti isinase, mkato wa kawaida bila mtindo wowote.

ii) Mwanafunzi haruhusiwi: kusuka nywele, kutinda nyusi.Kupaka wanja, kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kuvaa bangili, hereni, mikufu, pete au urembo wowote na vipodozi.

iii) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote anapokuwa katika mazingira ya shule na katika mikusanyiko maalumu ya kitaifa na ya kishule. Sare zivaliwe vizuri wakati wote, Shati/T – shirt lichomekewe vizuri ndani ya sketi. Mwanafunzi anayevaa sare ya shule isiyokidhi vipimo vilivyoelekezwa na Shule atadhibiwa na atalazimika kushona /kununua nyingine. Nguo za michezo zitavaliwa siku **maalum** za michezo.

iv) Mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo, kutotupa ovyo takatakaza aina yoyote darasani au nje ya darasa, kutokatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.

v) **Mwanafunzi haruhusiwi** kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo za shule bila ruhusa ya mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.

**E. MAHUDHURIO**

i) Mwanafunzi ambaye hatahudhuria masomo kwa zaidi ya siku mbili (02) mfululizo kwa sababu yoyote ile, haruhusiwi kuhudhuria masomo mpaka aapate kibali kutoka **IDARA YA TAALUMA.** Vilevile mwanafunzi ambaye hatahudhuria masomo kwa jumla ya siku tano (05) bila taarifa kabla ya mtihani wowote wa shule, hataruhusiwa kufanya mtihani huo.

ii) Kila mwanafunzi anawajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ya mchepuo wake pamoja na kipindi cha DINI.

**F. SIMU NA VIFAA VYA KI – ELECTRONIKI**

Mwanafunzi **HARUHUSIWI** kumiliki na/au kutumia simu, IPOD au kifaa chochote cha Electroniki akiwa shuleni. Mwanafunzi akikamatwa na simu, IPOD au kifaa cha electroniki Kisichoruhusiwa ataadhibiwa na kifaa kitachukuliwa na kuharibiwa. Mawasiliano ya mwanafunzi na mzazi yanafanyika kwa kutumia simu ya shule **namba 0618-086-660 na si vinginevyo.**

**2.3. Makosa yafuatayo yaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;**

a) Wizi.
b) Uasherati, ushoga, ulawiti na usagaji.
c) Ubakaji.
d) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
e) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
f) Kuoa au kuolewa.

g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
i) Kudharau bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha ya Taifa.
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
l) Kukataa adhabu halali.
m) Kutoroka vipindi, kutoroka shuleni, utoro wa muda mrefu bila taarifa.
n) Makosa ya jinai.

**2.4. Mambo muhimu ya kuzingatia na yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni :**
a)"Medical examination form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Kila mwanafunzi anaporipoti shuleni alete "Photocopy" ya cheti cha kuzaliwa au "Affidavit form"toka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kama hana cheti cha kuzaliwa.
d) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
e) kila mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuhitimu shule (leaving certificate) na result slip.
f) mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala katika bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.
g) mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule.(msiba au ugonjwa)
h) kwa kuwa mwanafunzi harusiwi kuwa na simu, mzazi unatakiwa kutumia simu zilizoorodheshwa hapo juu ya fomu.

**2.5. MICHANGO YA SHULE:**
(a) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi/mlezi ni:

| Na. | AINA YA MCHANGO | KIASI CHA FEDHA (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 45,000/= kwa mwaka |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= kwa mwaka |
| 3. | Ukarabati wa samani | 20,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| 5. | Nembo | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

NB: Fedha ya tahadhari haitarejeshwa. Pesa ya kitambulisho na Nembo zitapokelewa shuleni na kukabidhiwa kwa mhasibu wa shule.

**BIMA YA AFYA KWA MWANAFUNZI (NHIF)**

Kwa mwanafunzi asiye na kitambulisho cha Bima ya afya anatakiwa kuja na Tsh: 50,400/= (cash) na kuikabidhi kwa mhasibu wa shule kwa ajili ya kupewa Bima hiyo.

Fedha zote za michango ya uendeshaji wa shule, ukarabati wa samani na Tahadhali zilipwe kupitia akaunti ya shule yenye namba **30301200374 NMB,** Jina la akaunti ni **MOREMBE SECONDARY SCHOOL.**

**2.6. MAHITAJI MENGINE**

(i) Ream mbili (2) kwa mwaka iwe **double A** pamoja na flat file moja kwa kila mmoja.

HKL waje na mfagio wa nje (chelewa), leki, dawa ya chooni lita 5 aina ya dawa Dexi, squizer ya kukaushia maji.

HGK waje na mfagio wa nje (chelewa), mfagio wa ndani (soft broom), jembe lenye mpini, brash ndogo ya chooni.

HGLi waje na mfagio wa nje (chelewa), hard broom, fyekeo, dawa ya chooni lita 5 aina ya dawa Dexi.

**2.7 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Daftari kuanzia Quire 3 - ziwe 07

2. Begi la kubebea vifaa vya shule

3. Bofa, rula, kalamu za wino na penseli.

**2. 8 ORODHA YA VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI VINAVYOHITAJIKA**

Mwanafunzi ajitahidi apate angalau nakala moja ya vitabu vinavyo endana na mtaala mpya wa elimu kwa kila somo. Kumbuka kamusi ya Kiswahili na kiingereza ni muhimu.

**3.0 VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU VIRUDISHWE SHULENI BAADA YA KUJAZWA KIKAMILIFU**

a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Fomu ya wazazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**3.1 MENGINEYO:**

Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi yanategemea zaidi Mzazi/Mlezi. Ni imani yetu kuwa utampa mwanao msaada wa kila aina ili aweze kusoma kwa makini na kwa ufanisi.

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya kwa utekelezaji fanisi.**

**MWISHO**

Uongozi wa Shule unakutakia maandalizi mema ya kujiunga na shule ya sekondari **Morembe.** Ni Matumaini yangu utazingatia kanuni na sheria za shule ili lengo lililokuleta shuleni likamilike.

**KARIBU SANA MOREMBE SEKONDARI**

........................

**RAPHAEL M. KATIKIRO**

**MKUU WA SHULE**

# FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI KWA MWANAFUNZI.

Mkuu wa Shule,
Morembe Shule ya Sekondari
S.L.P 128
**MUSOMA.**

**Kwa mwanafunzi.**

Mimi……………………………………………………………………….. ninakubali nafasi niiyopewa kuingia Kidato cha…………… mwaka…………………. Katika shule ya Morembe Sekondari.

Naahidi kwamba:

1 . Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma.
2. Nitafanya bidii katika masomo na shughuli zote za shule.
3. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wowote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Morembe Sekondari. **MUNGU NISAIDIE:**

Sahihi ya mwanafunzi………………………………….. Tarehe……………………………………………

**KWA MZAZI/MLEZI:**

Mimi(Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………..
Mzazi/Mlezi wa……………………………………………………….

Naahidi kwamba:

1 . Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule
2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu
3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (homework) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni.
4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake.
5. Nitashirikiana na walimu kumweleza mwanangu maana ya shule na umuhimu wa kuwepo shuleni.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………..….. Tarehe………………………

PICHA

# FOMU YA USAJILI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)

**A: IJAZWE NA MWANAFUNZI**:

1 . Jina kamili la mwanafunzi …………………………………………....
2. Taifa……………………………
3. Uraia……………………………………..
4. Dini………………………………………..
5. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………
6. Mahali alipozaliwa………………………… Wilaya………………..Mkoa……………..
7. Shule ya sekondari aliyosoma……………………………………………………………………....
8. Tarehe ya kutoka shule aliyosoma……………………………………………..
9. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
1 0. Cheti cha kumaliza kidato cha nne (Leaving certificate)
1 1 . Nakala ya matokeo (Result slip kidato cha nne)

**B: MAELEZO BINAFSI YA MZAZI /MLEZI:**

1 . Jina kamili…………………………………………..
2. Anuani kamili ………………………
3. Sehemu unayoishi ……………………………………...
4. Mtaa…………………………………………………………………………..
5. Namba ya nyumba……………………………………………………….
6. Simu ya mkononi: Baba……………………………, Mama……………………………,
Mlezi…………………………..

**C: MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/ MLEZI:**

1 . Jina la mwajiri na Idara……………………………………………………….
2. Anuani yake……………………………… Simu namba………..…………….
3. Kazi ya mzazi/ Mlezi (Meneja, Daktari, Mfanyabiashara n.k)……………………..

**D: SOMO LA DINI**

Mimi…………………………………………………ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi.......................................................... Kidato cha………………… Ninaruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya ……………………………… Dhehebu la …………………………. siku ya Jumanne akiwa shuleni Morembe sekondari.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi…………………………….………

**MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL.**
**MOREMBE SECONDARY SCHOOL.**
**P.O. BOX 128,**
**MUSOMA-TANZANIA** **Form number……**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

---

Full name:……………………………………………………………………………………………………..
Age:………………………………………Height (in Cms)……………………………………………….
1.Blood Count………………………………….(Red and White)………………………………………..
2. Stool Examination ……………………………………………………………………………..
3. Urinalysis…………………………………………………………………………………………………….
4. Syphilis and other V.D………………………………………………………………………………..
5.T.B and Leapers Test………………………………………………………………………………..
6.Eye Test…………………………………………………………………………………………………….
7.Ear Test……………………………………………………………………………………………………..
8.Chest Test…………………………………………………………………………………………………
9.Adnominal Test……………………………………………………………………………………………..
10.Plano Test………………………………………………………………………………………………….
11. Spleen……………………………………………………………………………………………………
Addition information e.g Physical defects or impairments, infections chronic or family disease (e.g. Sickle-cell) Inability to eat certain foods e.t.c.
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
I certify that the above named Student is fit/ is not fit to pursue Secondary Education.
Signature……………………………………… Date…………………………………….
Station …………………………………………… ………………………………………
Official Stamp